JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KAHAWA TANZANIA

19 Juni 2024

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Bodi ya Kahawa Tanzania itauza kwa njia ya mnada wa hadhara vifaa chakavu yakiwemo magari, mitambo, samani za ofisi, vifaa vya TEHAMA na vifaa vingine katika mikoa ya **Kilimanjaro, Dar es Salaam,** na **Tanga**.

Maelezo zaidi ya vifaa hivyo ni kama yanavyoonekana hapa chini.

| Na. | Kituo | Anuani | Kifaa | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kilimanjaro | Bodi ya Kahawa Tanzania<br>Kahawa House<br>09 Br. J.K Nyerere<br>S.L.P 732<br>25101 Mawenzi<br>Moshi<br>Kilimanjaro | • Gari (Toyota Land Cruiser, Station Wagon)<br>• Jenereta (Wellux KVA=30, Volts240/415)<br>• Vifaa vya Tehama<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa mchanganyiko<br>• Samani za ofisi | 2 Julai 2024 |
| 2. | Dar Es Salaam | Kurasini/ Barabara ya Bandari<br>S.L.P 3437<br>Dar es salaam. | • Vifaa vya Tehama<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa mchanganyiko<br>• Samani za ofisi | 12 Julai 2024 |
| 3. | Tanga | Eneo la GOFU VIWANDANI<br>S. L. P 5946<br>Tanga | • Gari (Scania)<br>• Mitambo (Folk lift)<br>• Vifaa vya Tehama<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa mchanganyiko<br>• Samani za ofisi | 5 Julai 2024 |

## MASHARTI YA MNADA

1. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
2. Malipo ya vifaa chakavu ni asilimia mia moja (100%) na mteja atatakiwa kuondosha vifaa chakavu alivyonunua siku ya mnada.
3. Mnunuzi wa gari na mitambo atalazimika kulipa papo hapo amana “deposit” isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya bei na atatakiwa kukamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari na mitambo atatakiwa kuondoa/kuchukua mali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada husika kuanzia saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00).
6. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00) katika kituo kama ilivyoorodheshwa hapo juu.

**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KAHAWA TANZANIA**